



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



MWALIKO KWA WATAZAMAJI WA NDANI WA

UCHAGUZI MDOGO JIMBO LA AMANI ZANZIBAR NA KATA KUMI NA
MBILI ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Amani Mkoa wa Mjini Magharibi Tanzania Zanzibar na Udiwani katika Kata 12 za Tanzania Bara tarehe 17 Desemba, 2022. Kata zitakazofanya Uchaguzi Mdogo ni Kata ya Majohe katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dabalo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Ibanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mndumbwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Njombe Mjini katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, Misugusugu katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Dunda katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Kalumbeleza katika Halmshauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Mwamalili katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Mnyanjani katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, Lukozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na Vibaoni katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili Watazamaji wa Uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo Jimbo la Amani na Kata 12 za Tanzania Bara. Asasi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo zinatakiwa kuwasilisha maombi kwa kutumia mfumo wa usajili wa watazamaji (Observer Management System - OMS) kwa kutumia "link" ifuatayo <https://oms.nec.go.tz>.

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo-

- i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
- ii. Mahali sehemu ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi;
- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. Sehemu ambazo asasi au taasisi inataka kufanya zoezi hilo la utazamaji;
- v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao;
- vi. Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili wa taasisi au asasi;
- vii. Ikiwa taasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, wawili lazima wawe Watanzania;
- viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09 Novemba, 2022.

Imetolewa leo tarehe 3 Novemba, 2022 na:



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI